

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI - (VETA)



**MAKUBALIANO YA MKATABA WA KAZI ZA UJENZI WA CHUO CHA
WILAYA CHA VETA MKINGA**

A. Leo tarehe 02/06/2022 makubaliano yamefikiwa

KATI YA

Mkuu wa Chuo, VETA Tanga, S.L.P. 1204, Tanga, ambaye anaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802, Dodoma (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA


BASHIRU S. KAJEMBE wa TANGA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine kwa ajili ya kufanya kazi kama ilivyoorodheshwa hapa chini.

B. KAZI ZITAKAZOFANYIKA:

S/N	AINA YA KAZI
1	Kupaka rangi majengo (17) kwa kuta za ndani na nje, dari na facial board
2	Kujenga makaro ya zege ya kunawia mikono, kuoshea vyombo na kufulia nguo, kujenga ngazi (Steps) na kuweka mbao za kuandikia madarasani.

C. MAKUBALIANO YA MKATABA

- Gharama ya ufundi ni Shilingi za Tanzania 20,498,105.00 (Milioni ishirini mia nne tisini na nane elfu mia moja na tano tu).
- Kazi itafanyika katika kipindi kisichozidi siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe 6 Juni, 2022.
- Malipo yatafanyika kulingana na hati ya kazi (interim certificate) itakayotolewa na Mhandisi msimamizi wa mradi baada ya kazi kukamilika na kuthibitishwa.



vi) Malipo yatakatwa fedha za matazamio (Retention money 5%) na Fedha za zuio (Withholding tax on service 5%)

vii) Kazi itakayokuwa chini ya kiwango kilichokubaliwa (Sub Standard work) haitalipwa.

D. MSIMAMIZI WA UJENZI

Mwajiri atakuwa na haki ya kuweka Msimamizi wa ujenzi ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za ujenzi kwa niaba ya Mwajiri. Fundi au Mwakilishi wa Fundi Mkuu anatakiwa kutoa ushirikiano kwa Msimamizi wa ujenzi katika kutimiza majukumu yake.

E. KUVUNJWA KWA MKATABA

E.1 Iwapo Fundi Mkuu au mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajhusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya mradi;

E.2 Iwapo Fundi Mkuu au mafundi wake watafanya kazi bila kufuata maelekezo kutoka kwa Mhandisi Mshauri na kutozingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi zao;

E.3 Mwajiri kutomlipa Fundi ndani ya siku kumi na nne baada ya muda ambao angepaswa kumlipa.

F. USULUHISHI WA MIGOGORO

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi (arbitration).



